

**SHERIA YA UTOAJI WALESENI ZA BIASHARA,
(SURAYA 101)**

KANUNI

(Zimetengenezwa chiniya kifungu cha 29(1))

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNIZA UTOAJI WA LESENI ZA BIASHARA
ZA MWAKA 2026

Jina na tarehe
ya kuanza
kutumika

TS. Na.
626 la 2023

1.-(1) Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisha ya Kanuniza Utoaji wa Leseni za Biashara za mwaka 2026 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara za mwaka 2023 ambazo hapa zitarejewa kama “Kanuni kuu”.

(2) Kanuni hizi zitaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2026.

Marekebisha ya
kanuni ya 3

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3
kwa-

(a) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (1)
kanuni ndogo ifuatayo:

“(2) Maombi ya leseni mpya chini ya kanuni
ndogo ya (1) na maombi ya kuhuisha leseni
ya biashara yataambatishwa na taarifa
zifuatazo:

(a) uthibitisho wa matumizi ya
mfumo au vifaa vya kupokea
malipo kwa njia ya kidigitali,
ikijumuisha lipa namba au
TANQR;

(b) uthibitisho wa umiliki wa akaunti
ya benki kwa maombi
yanayohusu leseni ya biashara ya
madini, mifugo, mazao, mbao au
uvuvi; na

(c) taarifa nyingine yoyote
itakayohitajika na mamlaka ya

utoaji wa leseni kwa mujibu wa
sheria yoyote.”; na
(b) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (2) kuwa
kanuni ndogo ya (3).

Dodoma,
30 Juni, 2026

JUDITH SALVIO KAPINGA,
Waziri wa Viwanda na Biashara